JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Namba za simu Mkuu wa shule:
0783-556-699/0752-142850
Makamu Mkuu wa shule: 0688-622-762
Matron: 0742-378-068
Walimu wa Taaluma: 0764-547-728

Website: www.Dakawasec.sc.tz
E-mail: dakawahighschoool@gmail.com
E-mail: janemtindya@gmail.com

Shule ya Sekondari Dakawa,
S.L.P. 414,
MOROGORO

Tarehe: .....

Kumb. Na: DHS/E.10/18/.....

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:
.....
S.L.P.....
.....

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DAKAWA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO
MWAKA 2021/2022

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka wa masomo 2021/2022 tahasusi ya ..... Shule ya Sekondari Dakawa ipo umbali wa kilometa 65 kutoka Morogoro mjini katika barabara kuu iendayo Dodoma. Kwa wanaoingia Morogoro mjini kutoka nje ya mji wa Morogoro, washuke stendi kuu ya mabasi ya mikoani ***(Msamvu)*** na wapande gari za kwenda Dumila. Nauli ni Tsh. 3,000/= tu. Ukishapanda gari hilo utashukia kituo cha ***NJIA PANDA YA VETA – DAKAWA***. Ukishuka hapo utapata usafiri wa pikipiki utakaokupeleka moja kwa moja shuleni Dakawa High School kwa gharama ya Tshs. 2000/= tu, kwa umbali kilomita sita (6)
NB. Usitumie usafiri wa Tax kutoka Morogoro mjini ili kuepuka usumbufu wa malipo.

Kwa wanafunzi wanaoingia kwa barabara kuu itokayo Dodoma-Morogoro, wateremkie sehemu iitwayo ***NJIA PANDA YA VETA-DAKAWA,*** kisha wapande pikipiki na kushuka Kituo cha ***HIGH SCHOOL***, kwa nauli ya shilingi 2,000/= tu.

MWISHO WA KUTEREMKA HAPO NI SAA 10.00 JIONI KUTOKANA NA USALAMA.

Ni lazima mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na Result Slip.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/07/2021 Tarehe ya kuripoti wanafunzi wote wa kidato cha tano ni tarehe **03/07/2021 Mwisho wa kuripoti** ni wiki mbili baada ya tarehe ya kuripoti na baada ya hapo nafasi yako atapewa mtu mwingine.

2.0 **Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

2.1 **Sare za shule**.

a) Sare ya darasani;

Suti nyeusi pea mbili (2) zilizoshonwa kwa kitambaa cheusi gredi wani. Sketi iwe na urefu unaofikia kwenye kifundo cha unyayo wa mguu, iwe pana ya kutosha na isibane kwenye hips (mchoro wa mshono umeambatanishwa) NB: Koti liwe na kola.

Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na nusu kanzu yenye urefu wa kufika kwenye mfuko wa sketi na juba jeupe yenye urefu usiozidi urefu wa nusu kanzu.

Singlend (2) nyeupe (Aina ya Spider) za kuvaa ndani ya shati la shule

Sidiria tano (5) **nyeusi** na **nyeupe** tu ndizo zinaruhusiwa zisizokuwa na urembo wa aina yoyote.

Skin-tight tano

(5) Chupi 10

Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi au vinavyoitwa Juma na Roza vinavyopigwa rangi (kiwi)

Soksi pea tano (5) nyeupe za shule.

b) **Sare za michezo**:

Raba nyeupe.

Track mbili (2) ndefu nyeusi zisizobana maarufu kwa jina la baloteli (Aje na suruali tu, koti asilete)

Fulana (T-shirt) nyeupe (2) nzito aina ya Manga isiyo na kola. **Tafadhali asije na Fulana (T-shirt)nyepesi**)

c) **Sare ya prepo**:

Track-suti mbili (2) za Nembo ya Adidas rangi ya kijivu, nzito, zenye mistari myeupe pembeni (Material aina ya blanketi na siyo za kuteleza) **Koti lisiwe na kofia pia zisibane**.

d) **Sare za kushindia**:

Fulana (T-shirt)mbili (2) nzito aina ya Manga. 1 ya rangi ya kijivu na nyingine rangi ya njano ya kiini cha yai zisizokuwa na maandishi yoyote wala kola na zisiwe nyepesi

Sketi mbili (2) za dark bluu ndefu mpaka chini kwenye kifundo cha unyayo wa mguu zenye marinda ya kuelekea upande mmoja (sio linda box.)

Mitandio miwili (2); wa rangi ya njano na mweusi **isiyo na urembo** kwa wanafunzi wa kiislamu na kisiwe kitambaa cha mpira (Material).

NB: Fulana (T-shirts) zinapatikana shuleni zikiwa na nembo ya shule. Kwa maelelzo Zaidi piga simu shuleni.

d) MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI BILA KUKOSA.

Madaftari makubwa (counter Book Q3) - 8. Kwa ajili ya masomo ya Tahasusi. Madaftari madogo (yanayoanzia kurasa 200) - 8 kwa ajili ya mazoezi.

Ream 2 photocopy paper.

Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)

Scientific Calculator na Mathematical set (kwa wanafunzi wanaosoma Geography, Economics na BAM)

Cheti cha kuzaliwa

Hati ya matoke (Result slip)

Passport size za wazazi mbili na mbili za walezi. **(Muhimu sana)**

Taa ya solar atakayotumia kujisomea pindi umeme unapokatika.

e) Mahitaji kwa ajili ya chakula malazi:

Shuka za pinki pea mbili (2) spesho kwa wanafunzi. (Zisizo na urembo wowote) Foronya mbili (2) za pinki.

Mto mmoja (1).

Blanketi moja (1) zito.

Chandarua kimoja **(1) cheupe.**

Taulo, kitenge doti 1, nguo za kulalia mbili (2).

Vyombo vya chakula: sahani, bakuli, kikombe na kijiko viwe vya udongo au vya mfupa

f) Vifaa vya usafi:

Ni lazima kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo: -

Ufagio mmoja (1) wa chelewa mnene usio na mti kwa ajili ya kufagilia nje. Jembe (1) lenye mpini.

Rubber squizer 1.

Ndoo ndogo mbili (2) kwa ajili ya maji ya kunywa na kuogea.

Vifaa vingine kwa kila mkondo

Wanafunzi mchepuo wa **HGE** kila mmoja alete reki imara**.**

Wanafunzi mchepuo wa **HGK** kila mmoja alete Brash, (Toilet brush) ngumu ya kusugulia masinki ya vyoo yenye mshikio wa mti mfupi.

Wanafunzi mchepuo wa **HGL** kila mmoja alete hardbroom.

Wanafunzi mchepuo wa **HKL** kila mmoja alete fyekeo

2.2.0 **ADA YA SHULE KWA MWAKA**

S/N	AINA YA MALIPO	KIASI	BENKI/NAMBA YA AKAUNTI	JINA LA AKAUNTI
1	ADA	70,000/=	NMB 21801200076	DAKAWA SECONDARY SCHOOL

2.2.1 **MICHANGO MBALIMBALI**

S/N	**AINA YA MALIPO**	**KIASI**	**BENKI/NAMBA YA AKAUNTI**	**JINA LA AKAUNTI**
1	UKARABARI WA SAMANI	15,000/=	NMB 22101100133	MFUKO WA UZALISHAJI MALI DAKAWA
2	TAALUMA	20,000/=		
3	KUWALIPA VIBARUA	30,000/=		
4	HUDUMA YA KWANZA	5,000/=		
5	BIMA YA AFYA KWA WASIO NA NHIF	5,000/=		
6	FEDHA YA TAHADHARI	5,000/=		
7	MAFUTA NA MATENGENEZO YA GARI	20,000/=		
8	MAHAFALI	10,000/=		
	JUMLA	**110,000/=**		

2.2.2 **FEDHA ANAZOTAKIWA KUJA NAZO MKONONI**

MAELEZO	KIASI
Pesa ya Kitambulisho	5,000.00
Pesa ya nembo (mashati (2) ya shule)	2,000.00
Pesa ya picha (Passport size)	3,000.00
Pesa ya Tai	5,000.00
Pesa ya godoro	20,000.00
JUMLA	**35,000.00**

3. Sisi Walimu tunaamini kwamba mwanafunzi utajitahidi sana kuwa mwanafunzi *BORA* kwa: -

(i) Kuwa na nidhamu ya hali ya juu.
(ii) Kuzifahamu na kuzitii sheria za shule na za nchi.
(iii) Kujiheshimu na kuwaheshimu wanafunzi wenzako, walimu, wafanyakazi wasio walimu, viongozi wote na wananchi wa eneo letu.
(iv) Kushirikiana na wanafunzi wenzako, Uongozi wa shule, nchi na wananchi wote wanaozunguka eneo letu.
(v) Kujituma (bidii) katika kila jambo unalolifanya.
(vi) Kuwa Mdadisi/Mbunifu katika kujifunza na kuongeza maarifa zaidi pamoja na kuiga mambo mazuri na yenye manufaa katika masomo na maisha yako.
(vii) Kuwa nadhifu kimwili, kimavazi na utunzaji wa vifaa vya kazi na vifaa vyako vya kujifunzia na vya shule.
(viii) Kuwajibika katika masomo na kazi nyingine kwa mujibu wa sheria na taratibu za shule.
(ix) Kuwa mtiifu.
(x) Kuwa msikivu darasani na unapopewa maelekezo ya kazi ili uzifanye kwa usahihi.
(xi) Kujiamini uwapo darasani na kwa yale unayoyasema, kuuliza maswali, kujibu na kutoa ufafanuzi wa jambo lolote kwa ujasiri.

Kauli mbiu ya Dakawa sekondari ni hii:

"DAKAWA BILA DIVISION THREE INAWEZEKANA
TIMIZA WAJIBU WAKO."

MATEGEMEO YETU.

Jumuia ya Dakawa Sekondari inategemea kwamba mwanafunzi:
Utatumia muda wako wa miaka miwili vizuri kwa kujipanga kufaulu kwa Division I na II pekee; likiwa ndilo lengo kuu la Uongozi wa shule na jamii nzima ya shule ya sekondari Dakawa, hivyo:

(i) Utajiwekea malengo.
(ii) Utahudhuria vipindi darasani.
(iii) Utauliza maswali na kushiriki mijadala
(iv) Hutatoroka vipindi na kwenda kulala bwenini bila sababu maalum au sick room bila ED ya daktari.
(v) Utajisomea kwa bidii, hutasinzia darasani.
(vi) Utaandika nukuu za masomo (notes)
(vii) Utafanya mazoezi (exercises), majaribio (tests) na mitihani yote ya nje (external exams) na ya ndani (internal exams)
(viii) Utatafuta msaada kimasomo kwa walimu na wanafunzi wenzako kwa mada zitakazokusumbua.
(ix) Utatumia muda wako kwa uangalifu.
(x) Utazingatia sheria, kanuni na taratibu za shule.
(xi) Utajiheshimu na kuwaheshimu wengine.
(xii) Utaacha anasa zote ikiwemo matumizi ya simu.
(xiii) Usipofanya haya, maana yake unajiandaa kufeli au kufaulu kwa kubahatisha.

4. SHERIA ZA SHULE

(i) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii walimu wote, watumishi wasio walimu, viranja wa shule, viongozi wote na wanajamii wote na kujiheshimu wakati wote awapo Shuleni.

(ii) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu wanafunzi wenzake, ukumbi, mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k.

(iii) Anapaswa kuweka shule na eneo lake katika hali ya usafi wakati wote, bila kusahau usafi binafsi.

(iv) Mwanafunzi aheshimu kengele na awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.

(v) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani na wakati wa kijisomea.

(vi) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu wake.

(vii) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi, charger, line, earphone wala redio.

(viii) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kwa kutumiaa simu ya shule tu ambayo ni 0742-378-068.

(ix) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja, au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani.

(x) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu yake msikitini, kanisani, au hospitalini. Kama ndugu huyo ana maagizo afike ofisini aonane na uongozi wa shule.

(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.

(xii) Mafuta yenye harufu kali, perfume na spray, rangi za kucha, wanja, curl, nywele na mapambo kama bangili n.k haviruhusiwi kwa wanafunzi.

(xiii) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.

(xiv) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au kazi, wagonjwa watakaa chumba maalumu cha wagonjwa

(xv) Wanafunzi wanaruhusiwa kusuka nywele tano au saba pasipo kutumia nyuzi au nywele za bandia. Kwa wanao nyoa Wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni, urefu unaoruhusu kijiti cha kiberiti kikiwekwa kuonekana.

(xvi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.

(xvii) Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika katika eneo la mabwenini.

(xviii) Mwanafunzi haruhusiwi kuongeza na mtu yoyote ambaye si mwanajumuiya wa shule hii zaidi ya kusalimia.

(xix) Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa kumwombea ruhusa mwanafunzi kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

(xx) Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka kwa pamoja kwa usafiri uliondaliwa na shule. Hakuna ruhusa yoyote itakayotolewa mapema kabla ya siku rasmi ya kufunga shule.

(xxi) Mwanafunzi akiugua na kulazimika kwenda nyumbani kwa matibabu, Mzazi atawajibika kuja shule kumchukua na kumrudisha baada ya matibabu.

(xxii) Mwanafunzi ataletwa na Mzazi akichelewa kurejea kutoka likizo.

(xxiii) Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi zote za mikono kama vile anavyopaswa kuheshimu masomo yake, kila kipindi kilichopo kwenye ratiba ya kila siku ni muhimu.

(xxiv) Hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha maandishi kutoka katika Uongozi wa shule.

(xxv) Matusi ya aina yoyote ya kusemwa au kuandikwa havitakiwi shuleni na nje ya shule. Hii ni pamoja na kumtania mtu ambae hapendi kutaniwa.

(xxvi) Nguo rasmi za shule (sare) lazima zivaliwe wakati wote uhusikao. Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule bila nguo rasmi ya shule. Nguo fupi za kubana, pana kupita kiasi na mapambo ya aina yoyote havitakiwi kuvaliwa na mwanafunzi popote pale nje au ndani ya shule.

(i) MAKOSA YONAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE: -

i. Kutukana, kumpiga mwalimu au mtumishi mwingine yeyote.

ii. Kupigana na mwanafunzi mwenzake

iii. Kuoa au kuolewa.

iv. Utoro.

v. Biashara, ulevi na kutumia dawa za kulevya.

vi. Kuwa na mimba au kutoa mimba ndani au nje ya Shule.

vii. Kuingia na kushiriki kwenye vilabu vya pombe, sehemu za starehe, au nyumba za kulala wageni (Guest houses)

viii. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgono, au kuvuruga Amani na usalama wa watu shuleni.

ix. Kukataa adhabu itolewayo na mwalimu.

x. Kukataa kufanya mazoezi na mtihani bila sababu za msingi.

xi. Wizi

xii. Kudharau wimbo au bendera ya taifa.

xiii. Makosa ya jinai.

xiv. Kunyanyapaa wengine.

xv. Kuleta simu ya mkononi au kukutwa na viambatanishi vyake kama charger, betri, vocha, line, earphone n.k

xvi. Uasherati, ubakaji, ushoga, usagaji, na ulawiti.

xvii. Kukaa/kulala bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi za nje.

KARIBU SANA DAKAWA

.....
JANE MTINDYA

MKUU WA SHULE

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI



A. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:

1. JINA LA MWANAFUNZI: (MAJINA MATATU).....

2. TAREHE YA KUZALIWA: .....

3. MAHALI ALIPOZALIWA: WILAYA.....MKOA.....

4. MAHALI ANAPOISHI KWA SASA: MTAA..... KATA.....KIJIJI.....

   TARAFA: .....WILAYA: .....MKOA.....

5. JINA LA MWENYEKITI WA KITONGOJI/SERIKALI YA MTAA:.....

   NAMBA YA SIMU: .....

6. JINA LA BALOZI: .....NAMBA YA SIMU: .....

7. URAIA: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA: .....KABILA .....

8. SHULE NILIYOTOKA: .....

9. NAMBA YA MTIHANI (CSEE); .....SHULE NILIYOFANYIA MTIHANI KIDATO CHA NNE:

   .....WILAYA YA: .....MKOA: .....

10. DINI: .....DHEHEBU:.....

B *KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA.*

MIMI .....KIDATO CHA.....MWAKA.....MCHEPUO WA.....
Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa bila kutimiza kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.
TAREHE: .....SAINI: .....

C. *KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:* MWANAFUNZI:

Mimi: (MAJINA MATATU) .....SAINI: .....
nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria, kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai

yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

D. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI;(ANDIKA MAJINA MATATU)

1. JINA LA BABA: .....
   MAHALI ANAPOISHI MTAA/KIJIJI: .....KATA.....
   TARAFA..... WILAYA:.....MKOA:.....
   KABILA:.....KAZI YA BABA: .....
   SIMU YA BABA..... S.L.P.....MJI: .....
   YUKO HAI /AMEFARIKI .....
   ENDAPO UTABADILISHA NAMBA YA SIMU TOA TAARIFA SHULENI.

2. JINA LA MAMA: .....
   MAHALI ANAPOISHI MTAA/KIJIJI: .....KATA.....
   TARAFA:.....WILAYA:.....MKOA:.....
   KABILA:.....KAZI YA BABA: .....
   SIMU YA MAMA ..... S.L.P.....MJI: .....
   YUKO HAI /AMEFARIKI .....
   ENDAPO UTABADILISHA NAMBA YA SIMU TOA TAARIFA SHULENI.

   ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI:

3. JINA LA MLEZI WA KIUME..... MAHALI ANAPOISHI.....
   UHUSIANO.....SIMU: .....
   JINA LA MLEZI WA KIKE .....MAHALI ANAPOISHI.....
   UHUSIANO.....SIMU.....
   S.L.P. .....MJI.....
   NB. H**akikisha namba ya simu inapatikana muda wote na ni ya Mzazi / Mlezi**

E. MZAZI/MLEZI (AZAJE SEHEMU HII):

Mimi..... nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi.....na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri. Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo.

TAREHE: .....SAINI: .....

F: SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU:

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.
MAJINA MATATU. MFANO: ROSE ZABRON MUSSA

	JINA	UHUSIANO	NA. ZA SIMU	MAHALI NAPOISHI
1.	.....	.....	.....	.....
2.	.....	.....	.....	.....
3.	.....	.....	.....	.....
4.	.....	.....	.....	.....

PICHA YA BABA	PICHA YA MAMA	PICHA YA MLEZI NA. 1	PICHA YA MLEZI NA. 2

DAKAWA HIGH SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

NAME:..... AGE:.....DATE: .....

PERSONAL HISTORY

Is the examinee suffering from any of the following?
Indicate **YES** or **NO**

1. Tuberculosis.....
2. Pneumonia.....
3. Pleurisy.....
4. Asthma.....
5. Rheumatic fever.....
6. Allergic disorder.....
7. Heart disease.....
8. Gastric or duodenal .....
9. Recurrent indigestion.....
10. Jaundice.....
11. Dysentery.....
12. Varicose Veins.....
13. Kidney or Urinary Disease.....
14. Diabetes.....
15. Epilepsy .....
16. Deformity.....
17. Psychiatric.....
18. Eye disorder.....
19. Ear, Nose or throat disorder.....
20. Skin disease.....
21. Anemia.....
22. Gynaecological disorder.....
23. Malaria or other tropical disease.....
24. Cholera.....
25. Major or minor Operations.....
26. Serious accidents.....
27. Any other serious disorder.....

PHYSICAL EXAMINATION

1. Height .....
2. Skin disease.....
3. Weight.....
4. Eyes: Conjunctivae.....
5. Please state conditions of ears (if any discharge .....
   With glasses Right.....
   Left.....
   Abnomality.....
6. Cadiovascular system: .....
7. Blood pressure: Systolic .....Diastolic.....
   Heart: Any Murmer? .....
   Arteries and Veins.....
8. Abdomen.....
   Hydrocele.....
   Massess.....
   .....
   Liver.....
   .....
   Kidney.....
   .....
   Rectal.....
   .....
   ...
   Any clinical evidence of hyperacidity of gastric Duodenal ulcer?

Pupils……..
Vision Right…….
Vision Left…….

LABORATORY

1. Urine Albumin…… Sugar…… ….
   Lucocecytes…… Bilharzia…… …
2. Stool: Special emphasis on Hookworm or Bilhazias
3. Blood Examination: Hb level……
   (a) Neutrophils …… (d) Eosinophils……
   (b) Basophils…… (e) Lymphocytes…… …
   (c) Monocytes…… … (f) ESR……

4. X-ray examination – Chest……

5. Serology: Widal Test…… VDRL……

6. Pregnancy Test ……

CONCLUSION

I have examined Mr./Miss……
And consider that he/she is not physical/Mentally fit to be admitted to the Secondary School Studies.

…… …… ……
Date Signature Name

…… ……
Title Qualifications

Address: ……

……

……

……

ORODHA YA VITABU WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI.
IDARA YA KISWAHILI

1. VITABU VYA
   UCHAMBUZI
   USHAIRI
   JINA LA KITABUMWANDISHI.

Kimbunga	-	H. Goro M.S.
Fungate ya uhuru	-	Khatibu T.A.
Chungu tamu	-	Mvungi

RIWAYA.

Vuta n'kuvute	-	S.A. shafi
Usiku utakapokwisha	-	M. Msokile
Mfadhili	-	H. Tuwa

TAMTHILIYA

Morani	-	E. Mbogo P.
Nguzo mama	-	Muhando S.
Kivuli kinaishi	-	Mohamedi

2. **Kiswahili Sekondari** - kidato cha V & VI - Oxford.
3. **Kiswahili Sekondari – Kidato cha Tano (TIE)**
4. **Kiswahili Sekondari – Kidato cha Sita (TIE)**
5. **Kilangi E. Lucas (2019) Kiswahili 1 Shule za Sekondari Kidato cha 5 na 6**

ENGLISH DEPARTMENT

LANGUAGE – I -

1. Ashel, N. (2009) **Advanced Level English a Practical Approach**. DSM.
2. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form Six) - DSM
3. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form five) – DSM.
4. English Language for Secondary Schools, Language & Usage – Form Five & /six (TIE) papers.
5. Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.
6. Oxford advanced learners Dictionary-9th Edition

LANGUAGE –II-

1. Ashel, N. (2011), **Advanced Level Literature**. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.
2. **Advanced Level Literature**, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.
3. Achebe, A. (1966) **A man of the People**.
4. Ayi Kwei Armah (1968), **The Beautyful Ones Are Not Yet Born.**
5. Ibsen, H. (1882), **An Enemy of the People,** EA-DSM
6. Imbuga, FC (1976) **Betrayal in the City.**
7. Mirii Ngugi & Thing'ol (1982), **I Will Marry When I Want**, EAEP, DSM.
8. Institute of Education, **Selected Poems**.
9. Mloka, C. (2007) **The Wonderful Surgeon.**
10. English Language for Secondary Schools, Literature & Stylistics – Form Five & Six (TIE). Paper 2.

GEOGRAPHY DEPARTMENT

1. (Colin Buckle), **LANDFORMS IN AFRICA**

2. C.R. KOTHARI), **RESEARCH METHODOLOGY**
3. (H.C. TRURAN), **A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS**
4. (Goh cheng Leong.Gillian.C. Morgan), **HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY**

5. (DAVID WAUGH), **GEOGRAPHY-AN INTIGRATED APPROACH**.
6. (JOHN.M. PRITCHARD), **PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA**
7. (R.B. BUNETTE), **PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS FOR AFRICA.**
8.

READING LIST FOR HISTORY ONE.

1. Hallert, R. (1983). **Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers**. Nairobi, Kenya.
2. July, R.W. (1992). **A History of the African People**, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
3. Illife, J. (1995). **Africans, the History of the Continent**. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
4. Manning, P. (1990). **Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade**, Cambridge University Press.
5. Njiro, E. (1989). **A History of Africa in the 19th century**. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
6. Rodney, W. (1976). **How Europe underdeveloped Africa**, Publishing House, Dar es salaam, Tanzania.
7. Shillington, K. (2004). **History of Africa**. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.
8. Davidson, E. ef al (1997); The **growth of the African civilization East and Central Africa to thelate 19th century**, Longman Group Limited, Singapore.
9. Freud, B. (1998): **The making of contemporary Africa; The Development of African societiessince 1800**, Colorado, Lynne Rienner Publishers.
10. Kimambo, I and Temu, A (1969); **A History of Tanzania**, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
11. Robin, H. (1993); **African since 1875 A modern History**, East African Publishers Ltd., Nairobi, Kenya.
12. Roland, O. and Anthony, A. (2007). **Africa since 1800**, Cambridge University Press, New York, USA.
13. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
14. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)
15. History for secondary schools: Form Five (TIE)
16. History for Secondary Schools: Form Six (TIE)

READING LIST FOR HISTORY TWO.

1. Nelson throne **Essential modern world history**
2. **History of 21st century** (World history) (Oxford)
3. H.L. Peacock. **A History of Modern Europe 1789-1981** seventh Edition (2010)
4. **The History of Modern World** (2007) 6th Edition by Oxford University Press.

GENERAL STUDIES

1. Richard, R.F. Mbalase. **General Studies for Advanced Level Certificate**;
2. Mgaywa, B.M. **General Studies for Advanced level 3rd Ed**.
3. Joannes BigirwaMungu & Sospeter.M. Deogratias. **Understanding Advanced Level General Studies;** Advanced Secondary School Education;

BASIC APPLIED MATHEMATICS

1. Basic Applied Mathematics for Secondary School.
2. Basic Applied Mathematics Review.
3. Basic Applied Mathematics (TIE)

ECONOMICS REVISION BOOKS

1. Ambros Odhiambo (2018) Essentials of A- level Economics paper 1 (Form 5 & 6), First revised Edition, Current Syllabus
2. Ambros Odhiambo (2019) Essentials of A- level Economics paper 2 (Form 5 & 6), Current Syllabus

MISHONO YA SIKU ZA SIKUKUU.
Mchoro wa skati nyeusi
Mbele
Nyuma ina zipu.
Mchoro wa skati ya Dark blue
Mchoro wa koti Jeusi
Skati zaje ziskua na belt pana